

Kwa nini Muislamu haamini katika itikadi ya uhamaji wa roho (Tanasukh Al-Arwah)?

Kila kitu katika ulimwengu huu kiko chini ya udhibiti wa Muumba, Yeye pekee ndiye anayemiliki maarifa kamili, elimu kamilifu, uwezo, na nguvu ya kutii kila kitu kwa matakwa Yake. Jua, sayari, na magalaksi zinafanya kazi kwa usahihi tangu mwanzo wa uumbaji, na usahihi huu na uwezo unatumika kwa uumbaji wa wanadamu pia. Mshikamano uliopo kati ya miili ya wanadamu na roho zao unaonyesha kuwa haiwezekani kwa roho hizi kuishi katika miili ya wanyama au kutembea kati ya mimea na wadudu (uhamaji wa roho) au hata ndani ya watu wengine. Mwenyezi Mungu amempa mwanadamu akili na maarifa na kumfanya kuwa mwakilishi wake duniani, akamfanya kuwa bora na kumtukuzi juu ya viumbe wengi. Kwa hekima na uadilifu wa Muumba, kuna Siku ya Kiyama ambayo Mwenyezi Mungu atawafufua viumbe na kuwapima na kuwahukumu, na mwisho wao utakuwa Peponi au Motoni. Kila tendo jema au ovu litapimwa siku hiyo.

"Basi mwenye kutenda jema lenye uzito wa chembe ataiona** (7) **Na mwenye kutenda baya lenye uzito wa chembe ataiona" (Az-Zalzalah: 7-8).

سؤال وجواب حول الإسلام

Source: <https://e-quran.com/qa/sw/show/29/>

Arabic Source: <https://e-quran.com/qa/ar/show/29/>

Friday 3rd of April 2026 11:47:48 AM